# JARIDA LA

# CHUO KIKUU CHA SAYANSI NA TEKNOLOJIA MBEYA (MUST)

Toleo No. 03 | September 2025 | MUST



Follow us :

Mbeya University Of Science and Technology

# SALAMU YA MAKAMU MKUU WA CHUO



Prof. Aloys Ntanturo Mvuma
**Makamu Mkuu wa Chuo**

Karibu kwenye toleo hili la Jarida la MUST. Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kinaendelea kuwa nguzo ya maarifa, utafiti, na ubunifu. Ni fahari kubwa kushikishana nanyi mafanikio na maendeleo yaliyopatikana tangu toleo lililopita, tukidhihirisha dhamira yetu ya dhati ya kukuza ubora wa kitaaluma.

Miongoni mwa mafanikio makubwa ni kufanikisha kwa kiwango cha juu Kongamano la Kimataifa la FEW (Chakula–Nishati–Maji), ambalo lilikutanisha zaidi ya washiriki 200 kutoka nchi tisa barani Afrika pamoja na Marekani na Israel. Tukio hili limekuwa ishara ya mshikamano wetu katika kushughulikia changamoto shirikishi za usalama wa chakula, nishati endelevu, na usimamizi wa rasilimali za maji.

Katika kuendeleza sayansi na teknolojia, ubunifu unaendelea kustawi kwa kasi. MUST imepata hatimiliki (patent) ya dawa ya asili ya kuua wadudu kwa ajili ya kupambana na ugonjwa wa Banana Xanthomonas Wilt, hatua yenye umuhimu mkubwa katika kuendeleza kilimo nchini Tanzania. Hii ni fursa ya pekee ya kushirikiana na wadau, wabunifu, na washirika katika kupambana na changamoto za kilimo na kuendeleza suluhu endelevu.

Aidha, kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET), ujenzi wa miundombinu mikubwa unaendelea katika Kampasi Kuu na Kampasi ya Rukwa. Ujenzi huu unajumuisha majengo ya taaluma, maabara, karakana, na usimikaji wa samani, na kupanua uwezo wa MUST kutoa elimu na mafunzo bora kwa kiwango cha juu.

Kupitia mradi huohuo, zaidi ya wanataaluma 80 wamepata ufadhili wa kusomea Shahada za Uzamivu (PhD) na Uzamili (Master's). Hatua hii inalenga kujenga nguvukazi yenye ujuzi wa juu na kuhakikisha taifa linapata wataalamu bora wa baadaye.

Vilevile, MUST imeendelea kuwekeza katika ustawi na ujumuishi wa jamii yake kupitia programu mbalimbali za uhamasishaji. Hizi ni pamoja na elimu maalum, usawa wa kijinsia, mapambano dhidi ya UKIMWI, ukatili wa kijinsia, na afya ya akili. Hatua hizi zina lengo la kujenga mazingira salama, jumuishi, na yenye kuleta nguvu kwa kila mwanajumuiya.

Tunaposherehekea mafanikio haya, tunatoa shukrani za dhati kwa wafanyakazi, wanafunzi, wadau, na washirika wetu. Uaminifu, mshikamano na msaada wenu ndio msingi wa mafanikio haya. Pamoja, tunaendelea kuunda mustakabali wa MUST na kuchangia kwa dhati katika maendeleo ya taifa na uchumi wa maarifa duniani.

> Tusonge mbele kwa **mshikamano, dhamira**, na **nia** ya pamoja.

*Karibu!*

# YALIYOMO


01 UK. 04
MUST Yaongeza Ushirikiano wa Kimataifa Kupitia Makubaliano Rasmi na Chuo Kikuu cha NSAU – Urusi

02 UK. 06
MUST yasaini Mkataba wa Ushirikiano na Changelis Tanzania Ltd ya Ujerumani

03 UK. 08
Mwenyekiti wa Baraza la Chuo awapongeza viongozi waliomaliza muda wao wa uongozi.

04 UK. 09
Kampasi ya MTWARA mbioni kufunguliwa mwaka wa masomo 2025 / 2026

05 UK. 09
MUSTSO yapata Kiongozi mpya, aapiashwa rasmi aahidi uwazi

06 UK. 12
Serikali ya wanafunzi MUST yafanya ziara katika mradi wa HEET.

07 UK. 13
MUST yasaini mkataba wa Bilioni 1.9 manunuzi vifaa vya karakana na maabara za umeme kupitia mradi wa HEET

08 UK. 15
Walimu MUST wawezeshwa kutumia Teknolojia ya Moodle

09 UK. 17
MUST yapiga hatua kubwa katika utekelezaji wa mradi wa HEET

10 UK. 18
Chuo kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) cha shiriki maonyesho ya sita ya elimu ya juu Zanzibar.

11 UK. 19
MUST yafanya mazungumzo na Chuo Kikuu cha Sun Yat-sen kutoka China.

12 UK. 20
Semina ya wasimamizi wa mitihani yafanyika MUST kwa ajili ya maandalizi ya mitihani ya Juni 2025

13 UK. 21
Ujumbe wa Ubalozi wa Marekani watembelea MUST kuimarisha ushirikiano wa kielimu

14 UK. 24
Wadau wa FEW kutoka mataifa 9 duniani wakutana Mbeya kujadili mustakabali wa chakula, nishati na maji

15 UK. 26
Wanachuo MUST wahimizwa kuongeza juhudi zaidi katika ubunifu

16 UK. 27
Wadau wa kilimo na MUST waungana kukuza ujuzi wa wanafunzi kupitia mashamba darasa

17 UK. 29
Wataalamu wa Wizara ya Elimu, Sayanzi na Teknolojia watembelea miradi ya HEET-MUST

18 UK. 31
Wiki meneja 2025 yawavutia wengi.

19 UK. 34
Warsha kwa viongozi wa Chuo kukuza uwajibikaji, weledi na umoja

# MUST YAONGEZA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA KUPITIA MAKUBALIANO RASMI NA CHUO KIKUU CHA NSAU – *Urusi*



*Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), Prof. Aloys N. Mvuma (wa pili kushoto), akiwa kwenye picha ya pamoja na Dr. Vladislav Babin (wa kwanza kulia), Adv. Zuhura Shabani kutoka MUST (wa pili kulia) na Bi. Liubov Schmidt, Mkuu wa Idara ya Mahusiano ya Kimataifa wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Jimbo la Novosibirsk (NSAU), wakati wa ziara ya kutembelea maeneo mbalimbali ya chuo hicho nchini Urusi.*

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), kupitia Makamu Mkuu wake Prof. Aloys N. Mvuma na Mwanasheria wa Chuo Adv. Zuhura Shabani, kimefanya ziara rasmi ya kitaaluma katika Shirikisho la Urusi kuanzia tarehe 23 Juni 2025. Moja ya mafanikio makubwa ya ziara hiyo ilikuwa ni kusainiwa kwa makubaliano ya ushirikiano kati ya MUST na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Jimbo la Novosibirsk (NSAU).

Makubaliano hayo ni mwendelezo wa mahusiano ya kidiplomasia yaliyoanzishwa wakati wa ziara ya Balozi wa Urusi nchini Tanzania, Mheshimiwa Andrey Avetisyan, alipofika MUST mwezi Septemba 2024. Pande zote mbili zilitambua nafasi ya diplomasia ya elimu katika kuendeleza maendeleo endelevu na uvumbuzi.

Kupitia makubaliano hayo, MUST na NSAU wamekubaliana kushirikiana katika maeneo mbalimbali ikiwemo kubadilishana wanafunzi na wahadhiri, kufanya tafiti za pamoja, ushauri wa kitaalamu, pamoja na ushiriki katika warsha na mikutano ya kitaaluma. Pia wamekubaliana kubadilishana nyaraka za kitaaluma na kuandaa programu maalum za muda mfupi kulingana na vipaumbele vya taasisi zote mbili.

Mpango wa ubadilishanaji wa wanafunzi utaanza kutekelezwa rasmi katika mwaka wa masomo wa 2025/2026, ambapo kila chuo kitapokea wanafunzi kadhaa kwa mwaka. Wanafunzi watakaoshiriki watajiunga kwa muda mfupi kama wanafunzi wasiohitimu, wakifaidika na msamaha wa ada, ushauri wa kitaaluma na huduma muhimu kulingana na taratibu za taasisi mwenyeji.

Ushirikiano huu unadumisha historia ndefu ya mahusiano kati ya Tanzania na Urusi, yaliyoshamiri tangu enzi ya Muungano wa Kisovieti. Kwa hakika, baadhi ya miundombinu ya msingi ya MUST ilijengwa kupitia usaidizi wa kihistoria kati ya mataifa haya mawili.

Uratibu wa utekelezaji wa makubaliano haya utafanywa kwa pamoja na Ofisi ya Mahusiano ya Kimataifa ya MUST na Idara ya Miradi ya Kimataifa ya NSAU. Aidha, Prof. Mvuma alipata fursa ya kufanya mazungumzo ya ngazi ya juu na uongozi wa NSAU pamoja na kutembelea vituo muhimu vya utafiti na uvumbuzi, ikiwa ni pamoja na maabara za kisasa na teknolojia shirikishi.

Makubaliano haya yanadhihirisha dhamira ya MUST katika kukuza ushirikiano wa kimataifa kwa ajili ya kuboresha elimu ya juu, kuendeleza maarifa na kusaidia ajenda ya taifa ya ushirikiano wa kielimu na kidiplomasia ya maarifa.



Prof. Aloys N. Mvuma, Bi. Liubov Schmidt na Adv. Zuhura Shabani wakiwa kwenye moja ya karakana ya NSAU



Naibu Makamu Mkuu wa Chuo -Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu (DVC–ARC), Dr. Vladislav Babin (kushoto), Bi. Liubov Schmidt, Mkuu wa Idara ya Mahusiano ya Kimataifa (NSAU) wakiwa kwenye kikao cha uatambulisho kufuatia ziara ya Prof. Aloys N. Mvuma chuoni hapo.



Prof. Aloys N. Mvuma Makamu Mkuu wa chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) akiwa ameambatana na Bi. Liubov Schmidt, Mkuu wa Idara ya Mahusiano ya Kimataifa wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Jimbo la Novosibirsk (NSAU) wakiingia Ofisi ya Makamu Mkuu wa chuo NSAU nchini Urusi kwa utambulisho.



Prof. Aloys N. Mvuma (kulia), Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), akiwa na mwenyeji wake Prof. Evgenii Rudoi, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Jimbo la Novosibirsk (NSAU), wakati wa ziara rasmi ya kikazi nchini Urusi mnamo Juni 2025.

# MUST YASAINI MKATABA WA USHIRIKIANO NA CHANGELIS TANZANIA LTD YA UJERUMANI

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kimesaini makubaliano ya ushirikiano (MoU) na kampuni ya Changelis Tanzania Ltd, yenye makao makuu nchini Ujerumani, kwa lengo la kushirikiana katika miradi mbalimbali hususan kwenye sekta za elimu na mabadiliko ya tabianchi.

Makubaliano haya yamejikita katika maeneo ya kubadilishana ujuzi, utafiti na teknolojia, yakihusisha pia Chuo Kikuu cha Konstanz cha nchini Ujerumani. Kupitia mpango huu, MUST imepokea wanafunzi wa shahada ya umahiri katika usanifu majengo kutoka Ujerumani kwa ajili ya kujifunza na kushirikiana na jamii katika teknolojia bunifu ya ujenzi wa majengo kwa kutumia mianzi ya Tanzania.



*Mkurugenzi mtendaji wa kampuni ya Chengilis Tanzanaia Ltd, Bw, Roman Kreuzer, akitia saini ya makubaliano ya ushirikiano na Chuo Kikuu cha Sanyansi na Teknolojia Mbeya (MUST), yakishuhudiwa na wakili Zuhura Shabani.*



*Bw. Marc Dietric kutoka Chuo Kikuu cha Konstanz, Ujerumani , akiwasilisha mada kuhusu teknolojia ya ujenzi wa majengo kwa kutumia mianzi.*

Katika wasilisho maalum, mwanafunzi wa shahada ya umahiri katika usanifu majengo, Bw. Marc Dietrich, aliwasilisha utafiti na mbinu za ujenzi wa majengo kwa kutumia mianzi. Alieleza hatua mbalimbali zinazohusiana na uvunaji, uchakataji na uimarishaji wa mianzi ili iweze kutumika kwa usalama na ufanisi katika ujenzi wa nyumba na majengo ya kijamii.

Katika kipindi cha maswali na majibu, Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Aloys Mvuma, alihoji kuhusu usalama wa majengo hayo hususan katika majanga ya moto na mbinu zinazotumika katika kuezeka paa. Akijibu hoja hizo, Bw. Marc alibainisha kuwa suala la usalama limezingatiwa kwa kina kwa kutumia zege la saruji lililowekwa katikati ya mianzi pamoja na mfumo wa maji maalum wa dharura kwa ajili ya kuzima moto.

Prof. Mvuma aliwapongeza wanafunzi hao kwa ubunifu na umahiri, akisisitiza kuwa teknolojia hiyo ni ya manufaa makubwa kwa Tanzania kwa kuwa nchi ina utajiri wa malighafi ya mianzi. Aliongeza kuwa mradi huu utasaidia kupunguza gharama za ujenzi, kuongeza thamani ya bidhaa zinazotokana na mianzi, pamoja na kutoa ajira na maarifa mapya kwa jamii.

Baada ya wasilisho hilo, wanafunzi hao wakiwa pamoja na mhadhiri wao, Bw. Roman Kreuzer, walipata nafasi ya kutembelea miradi ya HEET katika kampasi ya MUST. Aidha, wataendelea kuwepo chuoni hapo kwa kipindi fulani ili kutoa elimu na mafunzo ya vitendo kuhusu ujenzi wa majengo kwa kutumia mianzi.



*Bw. Marc Dietric kutoka Chuo Kikuu cha Konstanz, Ujerumani , akionyesha jengo lililojengwa kwa kutumia Mianzi.*



*Makam Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya Prof. Aloys Mvuma akifuatilia wasilisho maalum kuhusu teknolojia ya ujenzi wa majengo kwa kutumia mianzi, lililotolewa na wataalam kutoka Chuo Kikuu cha Konstanz cha Nchini Ujerumani.*



*Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya MUST, Prof. Aloys Mvuma akiwa kwenye picha ya pamoja na Mkurugenzi wa Chengilis Tanzania ltd, Bw Roman Kreuzer, na wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Konstanz cha nchini Ujerumani mara baada ya hafla ya utiaji saini wa makubaliano ya ushirikiano.*



*Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Konstanz cha nchini Ujerumani, wakijiandaa kutembelea miradi ya ujenzi inayotekelezwa chini ya Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET).*

# MWENYEKITI WA BARAZA LA CHUO AWAPONGEZA VIONGOZI WALIOMALIZA MUDA WAO WA UONGOZI

Baraza la Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, menejiment na watumishi wa chuo wamefanya hafla fupi ya kuwaaga viongozi waliomaliza muda wao wa uongozi chuoni katika hafla maalumu iliyofanyika katika ukumbi wa Hotel ya Eden Highlands iliyopo jijini Mbeya. Viongozi hao ni Prof. Godliving Mtui ambaye alikuwa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma, Tafiti na Ushauri wa Kitalaamu (2019-2024) na Dkt. John P. John aliyekuwa Kaimu Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Mipango, Fedha na Utawala (2021-2024).

Akitoa hotuba kwenye hafla hiyo, Mwenyekiti wa Baraza Mhe. Zakia H. Meghji amemsifu Prof. Godliving Mtui kwa kazi nzuri ya kusimamia taaluma, utafiti na ushauri wa kitaalamu ambapo mpaka sasa taaluma chuoni imeimarika kwa kuongezeka kwa mitaala mipya inayokidhi mahitaji ya karne ya 21, pia kusisitiza wanataaluma kufanya tafiti mbalimbali ambazo zimesaidia kuinua hadhi ya chuo.

Kwa upande mwingine, Mwenyekiti alimshukuru Dkt. John P. John kwa juhudi zake za kusimamia ofisi ya Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anaesimamia Mipango, Fedha na Utawala licha ya kuwa umri wake ni mdogo lakini aliweza kusimamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo miradi ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali chuoni.

Kwa upande wake Makamu Mkuu wa Chuo Prof. Aloys Mvuma aliwashukuru viongozi hao kwa msaada mkubwa waliompatia wakiwa ni wasaidizi wake wakaribu zaidi. Akimzungumzia Prof. Mtui Makamu Mkuu wa Chuo alimsifu kwa kuwa mnyenyekevu wakati wote licha ya kuwa na uzoefu mkubwa, aliweza kujishusha na kufanya kazi kwa unyenyekevu mkubwa.

Akimzungumzia Dkt. John P. John Makamu Mkuu wa Chuo alimpongeza kwa ubunifu wake na uadilifu wake kwa kuwa ofisi aliyokuwa akiiongoza ina miradi mingi sana na fedha zote hupitia hapo, pia alimsifu kwa umahili wake wa kujifunza kwa haraka na kuijua ofisi kwa haraka licha ya kuwa aliipokea ofisi hiyo baada ya kifo cha aliekuwa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Fedha Mipango na Utawala marehemu Prof. Justinian Anatory.

Viongozi hawa wawili wamemaliza muda wao wa kuongoza kwenye nafasi zao na sasa wanaendelea na majukumu yao ya kitaaluma.



*Prof. Goodliving Mtui akipokea zawadi kutoka kwa Mwenyekiti wa Baraza, Mhe. Zakia Hamdani Meghji (katikati), kama ishara ya kutambua mchango wake baada ya kumaliza muda wake wa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu.*



Dkt. John P. John akipongezana na Prof. Goodliving Mtui katika hafla maalum ya kutambua na kusherehekea michango yao katika taasisi.



Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Mhe. Zakia Hamdani Meghji, akiwa kwenye picha ya pamoja na uongozi wa chuo na wawakilishi wa serikali ya wanafunzi.

# KAMPASI YA MTWARA MBIONI KUFUNGULIWA MWAKA WA MASOMO 2025 / 2026

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kimesaini mkataba wa ukarabati wa majengo kwa ajili ya Kampasi yake mpya mkoani Mtwara na kampuni ya Mahimbo & Company (T) Ltd. Mkataba huo wenye thamani ya zaidi ya shilingi za kitanzania milioni 700 ulitiwa saini katika ofisi ya Makamu Mkuu wa Chuo na kuhudhuriwa na viongozi waandamizi wa MUST pamoja na wawakilishi wa kampuni hiyo.



Wawakilishi wa Mahimbo Ltd pamoja na Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Aloys Mvuma, wakisaini rasmi mkataba wa ukarabati wa Kampusi ya Mtwara



Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Aloys Mvuma, akikabidhiana mkataba wa ukarabati wa chuo, Kampusi ya Mtwara, na Mhandisi Simon Mahimbo, Mkurugenzi Mtendaji wa Mahimbo Company Ltd.”

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Aloys Mvuma, alisisitiza uzalendo, ubora na uwajibikaji katika utekelezaji wa kazi hiyo. Alieleza kuwa mradi huo ni sehemu ya maagizo ya Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia chini ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014 (Toleo la mwaka 2023), inayolenga kukuza elimu ya ujuzi kupitia walimu wa amali.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Mhandisi Simon Mahimbo, alisema kuwa kampuni yake ina uzoefu wa zaidi ya miaka 10 katika sekta ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya serikali na taasisi za elimu hivyo anaamini wataifanya kazi hiyo kwa weledi wa hali ya juu. Aliahidi kutekeleza kazi kwa bidii na kwa kuzingatia matakwa ya mkataba.

Katika hatua nyingine Mkataba huu utahusisha ukarabati wa majengo mbalimbali ikiwemo ofisi, madarasa na mabweni ya wanafunzi ndani ya kampasi ya Mtwara.



*Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Aloys Mvuma, pamoja na wakilishi wa Kampuni ya Mahimbo na wataalamu wa Chuo wakijadiliana kabla ya kusaini mkataba wa ukarabati wa Kampusi ya Mtwara.*

Kampasi ya Mtwara inatarajiwa kuongeza fursa za elimu ya juu na ajira kwa wananchi, pamoja na kuongeza idadi ya walimu wa amali nchini, hivyo kuchochea maendeleo ya elimu ya ujuzi na kukuza uwezo wa wanafunzi kwa vitendo.

# MUSTSO YAPATA RAIS MPYA, AAPIASHWA RASMI AAHIDI UWAZI



*Rais mpya wa Serikali ya Wanafunzi wa MUST (MUSTSO), Bw. Yohana Lucas, akiapa kwa heshima*

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kimefanya hafla ya kuapisha rasmi rais mpya wa Serikali ya Wanafunzi (MUSTSO), Bw. Yohana Lucas, pamoja na Makamu wake Bi. Josephina Boha, tukio lililoshuhudia viongozi waandamizi wa chuo wakitoa nasaha muhimu kwa viongozi hao wapya wa wanafunzi.



*Bi. Josephina Boha akiapishwa kuwa Makamu wa Rais wa MUSTSO kwa muhula wa 2025/2026.*



*Rais wa Serikali ya Wanafunzi (MUSTSO) pamoja na Makamu wake wakiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi wa chuo baada ya kuapishwa kuongoza serikali ya wanafunzi kwa muhula wa mwaka 2025/2026.*

Katika hotuba yake baada ya kuapishwa, Rais mpya wa MUSTSO, Bw. Yohana Lucas, alitoa shukrani kwa uongozi wa chuo kwa kuwaamini na kuahidi kuwa ataongoza kwa misingi mitano muhimu: utawala wa uwazi na ushirikiano, uwakilishi wa haki, ushirikiano na menejimenti ya chuo pamoja na kukuza vipaji, ubunifu na ujasiriamali miongoni mwa wanafunzi.

Akiongea katika hafla hiyo Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Zacharia Katambara, aliwahimiza viongozi hao kuwa daraja la mawasiliano kati ya wanafunzi na uongozi wa Chuo na kuwaahidi kuwa uongozi wa Chuo utatoa ushirikiano wa moja kwa moja kwa serikali hiyo.

Kwa upande wake, Kaimu Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu, Dkt. Ramadhani Said Tekka, aliwakumbusha viongozi hao kuwa pamoja na nafasi waliyopewa, bado ni wanafunzi na wanapaswa kuzingatia kikamilifu kanuni, taratibu na sheria za chuo.

kwa upande wake rais wa serikali ya wanafunzi anaemaliza muda wake, Bw. Hemedi Bakari Ikoki, aliwapongeza serikali mpya kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi huku akisisitiza kuwa wanafunzi wana matarajio makubwa juu yao.
Hafla ni mwanzo mpya wa uongozi wa wanafunzi kwa mwaka wa masomo 2024/2025, huku matumaini yakiwa makubwa kwa viongozi wapya kusimamia haki, maendeleo, na ushirikiano chanya kati ya wanafunzi na chuo.

MUSTSO

# SERIKALI YA WANAFUNZI MUST YAFANYA ZIARA KATIKA MRADI WA HEET



*Viongozi wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUSTSO) wa mwaka wa masomo 2025/26 wakipokea maelekezo kutoka kwa wataalamu kabla ya kuanza ziara ya kutembelea Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) katika Chuo hicho.*

Uongozi wa serikali ya wanafunzi ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya uliingia madarakani mwaka huu na baadhi ya wanafunzi wamefanya ziara katika mradi wa ujenzi unaoendelea chuoni chini ya ufadhili wa HEET.

Akiongea mara baada ya kutembelea mradi huo, rais wa serikali ya wanafunzi Bw. Yohana Lucas, amesema kuwa lengo la kufanya ziara hiyo ni kujionea kazi inayoendelea hapa chuoni na pia kujifunza namna mradi huu mkubwa unayvotekelezwa na kusimamiwa na mkandarasi kutoka China na namna wataalamu wa ndani ya chuo wanavyoshiriki katika ujenzi huo.

Aidha, rais wa wanafunzi alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha anaipatia MUST fedha hizo kupitia mradi wa HEET na kuwa ni moja kati ya wanufaika wa mradi huo wa HEET. Pia alimpongeza Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya Prof. Aloys Mvuma kwa kusimamia vema mradi huo mpaka hapa ulipofikia kwani umefikia hatua nzuri na upo kwenye ubora.

Hata hivyo rais alivutiwa na ubunifu wa majengo na alisema wanafunzi watanufaika kwa karakana za kisasa na kumbi (venue) za kutosha na hivyo itapunguza vipindi vya usiku.

Pia rais wa serikali ya wanafunzi amewataka wanafunzi kutoka sehemu mbalimbali kujiunga na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kwani kuna miundombinu bora inayotosheleza pia kuna vifaa vya kisasa vya kujifunzia.

katika hatua nyinginerais ametoa rai kwa Uongozi wa Chuo kuamaliza ujenzi huo kwa wakati ili kuwezesha Chuo kudahili wanafunzi wengi zaidi na kusaidia vijana wanaohitimu masomo yao ya Sekondari kupata fursa ya kusoma MUST.

MUST inatekeleza ujenzi wa madarasa, kituo cha uhaulishaji teknolojia na karakana ikiwa ni juhudi za kuboresha miundombinu pia kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa chuoni hapa.



*Rais wa Serikali ya Wanafunzi (MUSTSO) pamoja na Makamu wake wakiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi wa chuo baada ya kuapishwa kuongoza serikali ya wanafunzi kwa muhula wa mwaka 2025/2026.*



*Viongozi wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUSTSO) wa mwaka wa masomo 2025/26 wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kumaliza ziara ya kutembelea Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET).*

# MUST YASAINI MKATABA WA BILIONI 1.9 MANUNUZI VIFAA VYA KARAKANA YA UMEME KUPITIA MRADI WA HEET

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kimeingia mkataba wa zabuni ya manunuzi ya vifaa vya karakana ya umeme chini ya Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET). Mkataba huu umeingiwa kati ya MUST na Mzabuni kutoka Morogoro, Kampuni ya Core Mult General Supply, ukiwa na thamani ya Shilingi 1,907,857,042.00.

Hafla ya kusaini mkataba huo imefanyika Chuoni MUST na kushuhudiwa na Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Zacharia Katambara na Bi Rukia Mkakile, Mkurugenzi wa kampuni ya Core Mult General Supply.

Akizungumza katika hafla hiyo, Prof. Katambara alisisitiza umuhimu wa utekelezaji wa mkataba huo kwa pande zote mbili huku akisisitiza kufanyika kwa kuzingatia muda uliokubaliwa wa miezi sita kuhakikisha kuwa Mzabuni anapeleka kwa wakati vifaa vyote huku vikiwa katika ubora unaotakiwa kama inavyoelezwa katika mkataba .



*"Tunatarajia kuona vifaa vyote vinakabidhiwa kwa wakati kama ilivyokubaliwa, na kuhakikisha vinakidhi viwango vya kitaalamu na kimataifa ili kuimarisha mazingira ya kujifunza kwa vitendo katika karakana ya umeme,"*

*alieleza Prof. Katambara.*



*Bi. Rukia Mkakile, Mkurugenzi wa Core General Supply Morogoro, akisaini mkataba wa usambazaji wa vifaa vya karakana ya umeme chini ya Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET).*

Kwa upande wake, Bi Rukia Mkakile alieleza kuwa kampuni yake iko tayari kutekeleza mkataba huo kwa ufanisi, kwa kushirikiana kwa karibu na MUST ili kuhakikisha mradi huu muhimu unakamilika kwa wakati na kwa ubora wa hali ya juu.

Mradi huu ni sehemu ya juhudi za serikali kupitia mradi wa HEET katika kuimarisha ubora wa elimu ya juu kwa lengo la kuongeza mchango wa vyuo vikuu katika kukuza uchumi wa taifa.




*Prof. Zacharia Katambara, Kaimu Mkuu wa Chuo, na Bi. Rukia Mkakile, Mkurugenzi wa Core Mult General Supply ya Morogoro, wakikabidhiana mkataba."*



*Picha ya pamoja baada ya makabidhiano ya mkataba: kutoka kushoto Bw. Keneth Runji, Bi. Mwamvua Ally, Bi. Rukia Mkakile, Prof. Zacharia Katambara na Bw. Disth Kibona."*

# WALIMU MUST WAWEZESHWA KUTUMIA TEKNOLOJIA YA MOODLE



*Dkt. Enerico John Sumbizi akiwaongoza washiriki waliohudhuria mafunzo ya matumizi ya takwimu kwenye Moodle .*

Kuanzia tarehe 8 hadi 11 Agosti 2025, Chuo Kikuu kiliandaa mafunzo maalum ya Moodle kwa wafanyakazi wanataaluma 25. Mafunzo haya ya ndani yalilenga kuwajengea uwezo walimu katika matumizi ya jukwaa la kidijitali la kujifunzia na kufundishia, ikiwa ni hatua muhimu katika safari ya chuo ya kuimarisha teknolojia ya kisasa katika elimu.

Mafunzo hayo yalifunguliwa rasmi na Kaimu Naibu Makamu wa Chuo Kikuu anayeshughulikia Taaluma, Tafiti na Ushauri wa Kitaalamu, Dkt. John P. John. Katika hotuba yake ya ufunguzi, Dkt. John alisisitiza umuhimu wa kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia yanayoendelea duniani.

> *"Chuo kimefanya jitihada kubwa kuweka mifumo ya kisasa ya kujifunzia na kufundishia ili kuendana na maendeleo ya kiteknolojia ya sasa," alisema. Aliwahimiza washiriki "kuwa makini na kujifunza kwa bidii ujuzi unaohitajika ili kubadilisha namna tunavyowasilisha elimu kwa wanafunzi wetu."*



*Washiriki wa mafunzo ya Moodle wakifuatilia kwa makini maelekezo kutoka kwa Dkt. Enerico John Sumbizi."*

Moodle, mfumo wa masomo wa kidijitali uliopewa kipaumbele katika mafunzo haya, ulielezewa kama chombo chenye uwezo wa kubadilisha kabisa mwenendo wa kufundisha na kujifunza. Washiriki walifundishwa namna ya kubuni au kusajili kozi, kuweka nyaraka za kufundishia, mihadhara, na video ambazo wanafunzi wanaweza kuzifikia kwa urahisi.

Pia walijifunza namna ya kuunda na kutathmini kazi za wanafunzi, kuandaa benki ya maswali, pamoja na kutengeneza mitihani na majaribio yanayoweza kusahihishwa moja kwa moja au kwa mkono. Mshiriki mmoja alikiri kwa kusema

,

*"Nimetambua Moodle siyo tu kwa ajili ya kupakia kazi, bali ni jukwaa la kuunda mazingira hai na rahisi ambapo wanafunzi wanaweza kujifunza kwa kasi yao, na sisi walimu tukawaongoza kwa ufanisi zaidi."*

Mafunzo yaliongozwa na Dkt. Sumbizi, Mkuu wa Idara ya Elimu ya Ufundi, ambaye alisisitiza mazoezi ya vitendo. Aliwaongoza washiriki hatua kwa hatua jinsi ya kusajili wanafunzi, kufuatilia maendeleo yao, na kutumia takwimu za Moodle ili kutambua changamoto za kitaaluma. Aidha, aliwaonyesha mbinu za kuongeza ushiriki wa wanafunzi kupitia mijadala ya mtandaoni, kura, na matumizi ya nyenzo za multimedia.

*"Moodle ikitumiwa vizuri huondoa pengo kati ya mwalimu na mwanafunzi,"* alisema Dkt. Sumbizi. *"Haibadilishi nafasi ya mhadhiri, bali huboresha namna ya kushirikisha, kupima, na kutumia maarifa."*

Mwisho wa mafunzo, washiriki walikuwa si tu wameongeza ujuzi wao wa kiteknolojia bali pia wamejenga kujiamini katika kutumia mbinu za kidijitali darasani. Wengi waliona mafunzo haya kama fursa ya kubadilisha mtazamo wao kuhusu nafasi ya teknolojia katika elimu. Mwalimu mmoja alisema,

*"Mafunzo haya yamenifungua macho juu ya fursa za ujifunzaji wa kidijitali. Nimehamasika kubadili kozi zangu ili wanafunzi wanufaike na mazingira yenye ushirikiano na unyumbufu zaidi."*



*Dkt. Enerico John Sumbizi akitoa mafunzo kwa wahadhiri mbalimbali juu ya matumizi ya teknolojia ya moodle.*

Kwa hakika, mafunzo ya Moodle hayakuwa tu warsha ya kujifunza mbinu mpya bali ni ushahidi wa dhamira ya chuo kukuza ubora wa taaluma kupitia ubunifu. Yameonyesha wazi dira ya chuo ya kuwaandaa walimu na wanafunzi kwa mustakabali wa elimu unaoendana na kasi ya maendeleo ya teknolojia duniani.



*Washiriki wa mafunzo ya Moodle wakifuatilia kwa makini maelekezo kutoka kwa Dkt. Enerico John Sumbizi."*




# MUST YAPIGA HATUA KUBWA KATIKA UTEKELEZAJI WA MRADI WA HEET



*Jengo la Taaluma lenye ghorofa nne katika Kampasi Kuu ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST). Jengo hili linajumuisha madarasa, maabara, na ukumbi wa mikutano wenye uwezo wa kuchukua watu 400, likijengwa chini ya ufadhili wa Mradi wa HEET.*

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kimeendelea kunufaika na utekelezaji wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (Higher Education for Economic Transformation – HEET), unaotekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Kupitia mradi huu, MUST imenufaika kwa kujengewa majengo makubwa ya kisasa katika kampasi zake mbili – Kampasi Kuu iliyopo Mbeya na Kampasi ya Rukwa – hatua inayolenga kuboresha miundombinu ya kufundishia, kujifunzia na kufanya tafiti za kitaaluma.



*Jengo la Karakana Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya Ndaki ya Rukwa*

Katika Kampasi Kuu, mradi wa HEET umejenga majengo matatu makubwa ambayo ni Jengo la Taaluma (Academic Block) lenye ghorofa nne, Kituo cha Ubunifu na Uhaulishaji wa Teknolojia (Centre for Innovation and Technology Transfer – CITT) lenye ghorofa nne, pamoja na Jengo la Karakana (Workshop) lenye vyumba 12 vya mafunzo kwa vitendo.

Mbali na ujenzi wa majengo hayo, mradi huu umeboresha miundombinu ya barabara, mifereji ya maji, njia za watembea kwa miguu, pamoja na mandhari ya mazingira kwa upandaji wa miti na majani, hatua inayolifanya eneo la chuo kuwa la kisasa na rafiki kwa mazingira.

Kwa mujibu wa Mratibu wa Mradi upande wa Miundombinu, QS Dkt. Japhari Shengeza, ujenzi wa jengo la taaluma katika kampasi kuu umefikia asilimia 97. Jengo hilo lina ukumbi wa mikutano wenye uwezo wa kubeba watu 400, maabara, na madarasa yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi kutoka 40 hadi 290 kwa darasa, na kwa mkupuo jengo linaweza kutumiwa na wanafunzi 3,340. Aidha, viti tayari vimeshafungwa katika madarasa yote.



*Jengo la Taaruma na ofisi mbalimbali Chuo Kikuu cha Sanyansi na Teknolojia Mbeya Ndaki ya Rukwa.*

Kwa upande wa jengo la CITT, lina uwezo wa kutumiwa na watumiaji 705 kwa mkupuo, na litakuwa kitovu cha ubunifu, teknolojia na ushirikiano kati ya chuo, sekta binafsi na jamii.

Katika Kampasi ya Rukwa, mradi huu unatekeleza ujenzi wa jengo la taaluma lenye ghorofa tatu lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,920 kwa mkupuo, pamoja na jengo la karakana lenye vyumba tisa vya karakana kwa ajili ya mafunzo ya vitendo kwa watumiaji 550 kwa mkupuo. Ujenzi wa majengo haya umefikia asilimia 98, na unajumuisha pia ujenzi wa barabara ya lami, njia za watembea kwa miguu, na maegesho ya magari.



*Jengo la Taaruma Chuo Kikuu cha Sanyansi na Teknolojia Mbeya Ndaki ya Rukwa.*

Kwa sasa, wakandarasi katika kampasi zote mbili wako katika hatua ya majaribio ya mifumo ya umeme, maji, na TEHAMA (ICT), ambapo inatarajiwa kuwa majengo yote yatakabidhiwa kwa matumizi ifikapo mwezi Oktoba mwaka huu.



*Jengo la Karakana Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojoa Mbeya kampasi kuu.*

Mbali na ujenzi wa miundombinu, mradi wa HEET pia umechangia katika kujenga uwezo wa kitaaluma kwa kutoa ufadhili wa masomo kwa watumishi 85 wa MUST, wakiwemo 58 wanaosoma shahada ya uzamivu (PhD) na 27 wanaosoma shahada ya umahiri (Masters) katika vyuo vikuu mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Utekelezaji wa mradi wa HEET katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) ni hatua kubwa kuelekea kuboresha ubora wa elimu ya juu, utafiti, ubunifu na mchango wa chuo katika maendeleo ya kiuchumi ya taifa, sambamba na dira ya serikali ya kujenga uchumi wa viwanda unaotegemea maarifa na teknolojia.



*Jengo la Kituo cha Ubunifu na Uhaulishaji wa Teknolojia (Centre for Innovation and Technology Transfer – CITT) Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST).*

HEET
HIGHER EDUCATION FOR ECONOMIC TRANSFORMATION

# CHUO KIKUU CHA SAYANSI NA TEKNOLOJIA MBEYA (MUST) CHA SHIRIKI MAONYESHO YA SITA YA ELIMU YA JUU ZANZIBAR.





*Washiriki kutoka MUST wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa Maonyesho ya Sita ya Elimu ya Juu Zanzibar katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Unguja, wakionyesha mshikamano na uwakilishi wa Chuo.*

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kimeshiriki katika Maonyesho ya Sita ya Elimu ya Juu yaliyofanyika Zanzibar kuanzia tarehe 14 hadi 20 Julai 2025 ambapo kimetunukiwa pia cheti cha kutambua ushiriki wake.

Maonyesho hayo yaliyobeba kauli mbiu isemayo "Elimu ya Juu ni Nguzo ya Mabadiliko: Tuikuze, Tuitumie, Tuhifadhi" yalifunguliwa rasmi na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Mhe. Lela Muhamed Mussa Katika viwanja vya Mnazi Mmoja

Mhe. Waziri Lela alitembelea mabanda ya washiriki ambapo aliweza kufika katika banda la MUST na kupongeza mchango mkubwa wa chuo katika sekta ya elimu ya juu pia alipongeza MUST kwa kushiriki kikamilifu katika maonyesho hayo pamoja na maendeleo makubwa yanayoendelea Chuoni huku akitaja ujenzi wa majengo ya ubunifu na karakana za kisasa chini ya Mradi wa mageuzi ya Elimu ya JuuHigher (HEET)

Waziri Lela alieleza kuwa jitihada za MUST katika kutoa elimu ya Sayansi na Teknolojia ni mfano wa kuigwa, na akasisitiza umuhimu wa vyuo vikuu kuendelea kushiriki katika maendeleo ya nchi kupitia elimu bora na bunifu.



*Mhe. Waziri Lela Mohamed Mussa pamoja na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Bw. Khalid Masoud, wakiwa wakimsikiliza Mhaziri Dkt. Phesto Peter Namanyara walipotembelea banda la Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) katika Maonyesho ya Sita ya Elimu ya Juu Zanzibar."*

kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali anayeshughulikia Utawala, Bw. Khalid Masoud Wazir, alieleza kuwa maonyesho ya mwaka huu ni ya sita tangu kuanzishwa kwake, na yameendelea kukua kwa kasi kubwa.



*Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Mhe. Lela Muhamed Mussa, akimkabidhi Cheti cha Ushiriki wa Maonyesho ya Sita ya Elimu ya Juu Zanzibar Mhaziri wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, Dkt. Phesto Peter Namanyara, katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Unguja-Zanzibar."*

# MUST YAFANYA MAZUNGUMZO NA CHUO KIKUU CHA SUN YAT-SEN KUTOKA CHINA.



*Prof. Aloys Mvuma akizungumza na Prof. Xia kutoka Chuo Kikuu cha Sun Yat-sen, China, kuhusu masuala ya ushirikiano wa kielimu na utafiti.*

MUST imefanya mazungumzo rasmi na ujumbe kutoka Chuo Kikuu cha Sun Yat-sen cha nchini China, ikiwa ni hatua ya awali kuelekea kuanzishwa kwa ushirikiano wa kimkakati katika nyanja mbalimbali za kitaaluma, utafiti na maendeleo. Mazungumzo hayo yalifanyika Jumanne, tarehe 8 Julai 2025 katika ofisi za Makamu Mkuu wa Chuo, jijini Mbeya.

Akizungumza wakati wa kuukaribisha ujumbe huo, Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Aloys Mvuma, alieleza utayari wa MUST kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sun Yat-sen katika kukuza ubadilishanaji wa maarifa, wanafunzi, na wataalamu. Alisisitiza kuwa chuo hicho cha China kinatambulika kimataifa kwa umahiri wake katika tafiti, ubora wa ufundishaji, na ubunifu wa kiteknolojia.

Majadiliano hayo yaliratibiwa na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu, Prof. Said Vuai, ambaye alihimiza pande zote mbili kubaini kwa pamoja maeneo yenye tija kwa ushirikiano wa pande mbili, ili kujenga msingi madhubuti wa uendelezaji wa elimu ya juu kwa manufaa ya nchi zote mbili.

Kwa upande wa Chuo Kikuu cha Sun Yat-sen, Prof. Xia alieleza kuwa taasisi hiyo ya umma iko Guangzhou na ni miongoni mwa vyuo bora nchini China, ikiwa na matawi matano katika miji mitatu. Alibainisha kuwa kutokana na uzoefu huo, chuo hicho kiko tayari kushirikiana na MUST katika maeneo ya ubobezi kama afya, kilimo, uhandisi na teknolojia ili kuimarisha elimu, utafiti na ubunifu.

Katika mazungumzo hayo, pande zote mbili zilifikia makubaliano ya kuandaa nyaraka ya awali (concept note) itakayobainisha maeneo mahsusi ya ushirikiano, na baadaye kuandaa rasimu ya mkataba wa makubaliano ya kimataifa (MoU). Rasimu hiyo itapitiwa kwa pamoja na kusainiwa rasmi kabla ya kuanza kwa utekelezaji wa programu mbalimbali za pamoja.



*Prof. Aloys Mvuma akipokea zawadi ya heshima kutoka kwa Prof. Xia wa Chuo Kikuu cha Sun Yat-sen; kushoto ni Prof. Said Vuai, akishuhudia tukio hilo.*



*Viongozi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) wakipiga picha ya pamoja na wawakilishi wa Chuo Kikuu cha Sun Yat-sen, China, baada ya kikao cha mazungumzo ya ushirikiano wa kielimu.*

Katika kuhitimisha kikao hicho, viongozi wa vyuo vyote viwili walisisitiza umuhimu wa kutumia nafasi hiyo kuendeleza uhusiano wa muda mrefu kati ya Tanzania na China, ambao ulianza tangu enzi za uongozi wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Miongoni mwa matunda ya ushirikiano huo ni ujenzi wa Reli ya TAZARA, kama mfano wa miradi mikubwa ya ushirikiano wa maendeleo kati ya mataifa hayo mawili.

# SEMINA YA WASIMAMIZI WA MITIHANI YAFANYIKA MUST KWA AJILI YA MAANDALIZI YA MITIHANI YA JUNI 2025




*Bw. William Matungwa akitoa mada katika semina ya wasimamizi wa mitihani kwa ajili ya Semester ya Pili, akisisitiza umuhimu wa uadilifu, uwajibikaji, na ufuatiliaji makini katika usimamizi wa mitihani.*

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kimeendesha semina maalum kwa wasimamizi wa mitihani kama sehemu ya maandalizi ya mitihani ya mwisho wa muhula wa pili mwaka wa masomo 2024/2025. Semina hiyo muhimu ilifanyika katika chuoni hapo na kuhudhuriwa na idadi kubwa ya watumishi wanataaluma ambao husimamia mitihani hiyo.

Akifungua rasmi semina hiyo, Dkt. Somo Mgaza Muya, Mkurugenzi wa Mafunzo ya Awali, aliwataka wasimamizi wote kusikiliza kwa makini maelekezo yatakayotolewa na kuhakikisha kuwa wanatekeleza majukumu yao kwa uwajibikaji wa hali ya juu. Alisisitiza kuwa semina hiyo ni fursa muhimu ya kujikumbusha taratibu na kanuni za usimamizi wa mitihani, sambamba na kujadili changamoto zilizojitokeza katika mitihani iliyopita.

Mkuu wa Idara ya Mitihani, Bw. William Matungwa, aliwasilisha mada yenye uzito kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu usimamizi wa mitihani. Aliainisha changamoto zilizobainika katika mitihani ya awali, akazungumzia kwa kina kanuni na miongozo ya usimamizi, na kusisitiza kuwa nidhamu na umakini wa wasimamizi ni msingi wa haki katika tathmini ya kitaaluma. Alibainisha kuwa jumla ya wanafunzi zaidi

ya 11,613 wamesajiliwa kushiriki mitihani ya muhula huu, hivyo ni muhimu kwa wasimamizi kuwa makini katika utekelezaji wa majukumu yao ili kuepusha dosari zozote zinazoweza kuathiri mchakato huo nyeti.

Katika kipindi cha mijadala, Dkt. Malunguja aliibua hoja kuhusu uteuzi wa wasimamizi wakuu na majukumu yao. Ilielezwa kuwa msimamizi mkuu huteuliwa na Rasi wa Ndaki husika, na jukumu lake ni kuratibu kwa karibu shughuli zote za usimamizi katika maeneo ya mitihani. Hoja hii ilifungua majadiliano ya kina kuhusu uwazi, mgawanyo wa majukumu na ushirikishwaji wa wahusika katika maandalizi ya mitihani.

Kwa upande wake Dkt. Hadija Matimbwa, Mkurugenzi wa Uthibiti Ubora wa Chuo, alichangia mjadala kwa kuahidi kufuatilia kwa karibu masuala yanayohusu stahiki za wasimamizi wa mitihani. Alisisitiza kuwa ufanisi wa wasimamizi unategemea pia mazingira bora ya kazi na kutambua mchango wao. Ahadi yake ilipokelewa kwa shukrani na washiriki wa semina hiyo, huku wengi wakionesha matumaini kuwa hatua hiyo itaboresha zaidi utendaji wao.

Semina hiyo ilihitimishwa kwa hotuba kutoka kwa Dkt. Muya, ambaye aliwahimiza wasimamizi wote kutumia maarifa waliyoyapata kwa weledi, uadilifu, na kuzingatia miiko ya kazi. Alitoa rai kwa kila mmoja kuwa mstari wa mbele katika kulinda hadhi ya chuo kwa kuhakikisha mitihani inafanyika kwa utulivu, weledi na kwa kuzingatia viwango vya kitaaluma.

Kwa ujumla, semina hii iliimarisha maandalizi ya mitihani ya Juni 2025, na kutoa fursa kwa wasimamizi kupata mwongozo wa pamoja wa utekelezaji wa kazi yao kwa ufanisi.

# UJUMBE WA UBALOZI WA MAREKANI WATEMBELEA MUST KUIMARISHA USHIRIKIANO WA KIELIMU



*Viongozi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) pamoja na wawakilishi wa Ubalozi wa Marekani nchini Tanzania kwenye picha ya pamoja mara baada ya kikao cha mazungumzo ya ushirikiano kilichofanyika katika ofisi ya Makamu Mkuu wa Chuo.*

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kimepokea ujumbe maalum kutoka Ubalozi wa Marekani jijini Dar es Salaam, hatua inayotazamwa kama mwanzo wa ushirikiano mpana wa kielimu kati ya pande hizo mbili. Ujumbe huo uliongozwa na Bi. Laura Shayo, Mkuu wa Idara ya Lugha ya Kiingereza katika Ubalozi wa Marekani, akifuatana na Bw. Christian Oganga, afisa kiunganishi wa ubalozi huo. Walipokelewa kwa heshima na Prof. Zacharia Katambara, Makamu Mkuu wa Chuo (Kaimu), ambaye aliwakaribisha katika majadiliano na menejimenti ya chuo.



Bw. Christian Oganga, & Ms Laura Shayo maafisa wa Ubalozi wa Marekani, waakitoa ufafanuzi kuhusu ushirikiano na fursa mbalimbali baina ya MUST, Ubalozi, na Vyuo mbalimbali kutoka nchini Marekani.

Katika mazungumzo hayo, wahusika walijadili maeneo kadhaa ya ushirikiano yenye umuhimu kwa MUST na kwa sekta ya elimu ya juu kwa ujumla. Miongoni mwa ajenda kuu zilizogusiwa ni programu za kubadilishana wanafunzi kati ya MUST na vyuo vikuu vya Marekani, uanzishwaji wa programu maalum za kitaaluma na kitaalamu, ushirikiano wa utafiti, pamoja na kuboresha lugha ya Kiingereza kwa wanafunzi na walimu. Ujumbe wa ubalozi ulisisitiza kuwa hatua hizi zitachangia si tu kuimarisha kiwango cha elimu chuoni, bali pia kuandaa wahitimu wenye ushindani katika soko la ajira la kimataifa.

Akizungumza kwa niaba ya ujumbe, Bi. Shayo alipongeza MUST kwa kujikita katika kukuza elimu ya sayansi na teknolojia nchini. Alisema kuwa elimu ni daraja linalounganisha tamaduni na mataifa, na kwamba kuunganisha MUST na vyuo vikuu vya Marekani kutafungua fursa pana za kubadilishana maarifa na kuendeleza ubunifu unaovuka mipaka. Naye Bw. Oganga aliongeza kuwa ubalozi umejipanga kusaidia miradi yenye tija na endelevu, hususan katika kukuza uwezo wa lugha ya Kiingereza na kujenga misingi imara ya tafiti za pamoja.



Bw. Christian Oganga, & Ms Laura Shayo maafisa wa Ubalozi wa Marekani, wakiwa kwenye kikao cha pamoja na viongozi mbalimbali wa Chuo.

Kwa upande wake, Prof. Katambara alishukuru kwa ziara hiyo na kusisitiza dhamira ya MUST ya kushirikiana kikamilifu katika miradi ya kimataifa. Alieleza kuwa ziara hiyo imekuja wakati muafaka ambapo chuo kipo katika mpango wa kupanua miundombinu na kuongeza kozi mpya. Kwa mujibu wake, ushirikiano wa kimataifa utakuwa nguzo muhimu ya kuhakikisha wahitimu wa MUST wanakuwa na ushindani wa kimataifa na tafiti zao zinagusa changamoto za kitaifa na za kimataifa.

Ziara hiyo pia imeelezwa kuwa inalingana na mkakati wa taifa wa kutumia elimu ya juu kama injini ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kwa MUST, ushirikiano huu unatarajiwa kupanua fursa kwa wanafunzi waliopo chuoni na kuwajengea walimu uwezo wa kitaaluma. Wataalamu wa elimu wanaona kuwa ushirikiano huu unaweza kuongeza nafasi za ajira, ubunifu na maendeleo ya kitaaluma, na hivyo kuifanya MUST kuwa na heshima si tu nchini Tanzania bali pia katika jukwaa la kimataifa.

Ziara hiyo ilihitimishwa kwa matarajio makubwa kutoka pande zote mbili kwamba majadiliano hayo yataleta makubaliano ya haraka na miradi ya pamoja. MUST imeahidi kutoa ushirikiano wa karibu ili kuhakikisha mawazo yaliyojadiliwa yanageuka kuwa miradi ya vitendo yenye manufaa ya moja kwa moja kwa wanafunzi na jamii. Kwa ujumbe wa Ubalozi wa Marekani, ziara hiyo ilikuwa ni uwekezaji wa kimkakati katika mustakabali wa viongozi wa kesho wa Tanzania.

# WADAU WA FEW KUTOKA MATAIFA 9 DUNIANI WAKUTANA MBEYA KUJADILI MUSTAKABALI WA CHAKULA, NISHATI NA MAJI




*Baadhi ya Washiriki wa Kongamano la FEW wakiwa kwenye picha ya pamoja na Meza kuu siku ya ufunguzi wa Kongamano.*

Mkutano wa Chakula-Nishati-Maji (Food-Energy-Water/FEW) Afrika Mashariki ulifunguliwa rasmi Julai 14 katika Hoteli ya Eden Highlands, ukiwaleta pamoja washiriki zaidi ya 200 kutoka nchi tisa kujadili suluhisho shirikishi kwa changamoto kubwa zinazoikabili kanda hii ya Afrika Mashariki.

Mkutano huo wa siku tatu uliandaliwa na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kwa ushirikiano na Shirika la CultivAid, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Chuo Kikuu cha Maryland (Marekani) na Taasisi ya Volcani ya Israel. Washiriki kutoka Tanzania, Kenya, Uganda, Ethiopia, Malawi, Zambia, Afrika kusini, Israel na Marekani walitumia wasaa huu kujadili kwa kina na kuibuka na suluhisho Madhubuti kwa maslahi mapana ya sekta ya maji, nishati na chakula.



*Washiriki wa Kongamano wa FEW wakijadiliana kwa pamoja katika makundi ili kupata Suluhu ya changamoto za Chakula, Nishati na Maji.*

Katika hotuba yake ya ufunguzi, Makamu Mkuu wa Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), Profesa Aloys N. Mvuma, aliwapongeza wajumbe kwa kufanikisha ushiriki wao na kusisitiza kuwa mkutano huo utatoa mchango mkubwa kwa sekta ya kilimo nchini Tanzania na duniani kwa ujumla. Alisema, mkutano huu umekuja katika wakatu muafaka ambapo Tanzania inalenga kuilisha Afrika kwa kuzalisha mazao mengi.

Alisisitiza pia juhudi za Serikali ya Tanzania za kusambaza umeme wa gharama nafuu hadi ngazi ya vijiji na mitaa, akitanabaisha kuwa mkutano huo unalenga kuonyesha namna rasilimali za nishati na maji zinavyoweza kuunganishwa ili kuongeza tija ya chakula, usalama wa chakula na faida endelevu.

Pia amesema, MUST kama chuo cha teknolojia kinaamini kwenye teknolojia kubuni na kutafiti njia za kusaidia sekta mbalmbali haswa kilimo cha umwagiliaji, badala ya kutegemea mvua kuzalisha kuzalisha kwa wingi.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Mh. Solomoni Itunda ambaye alikuwa mgeni rasmi, alisifu jitihada za MUST katika kuziba pengo kati ya tafiti na uzoefu wa moja kwa moja wa wakulima wa Kitanzania. Alisema kuwa katika maisha ya binadamu, mambo matatu ambayo ni nishati, chakula na maji ni muhimu. Aliongeza kuwa mkoa wa Mbeya unashika nafasi ya juu miongoni mwa mikoa mitatu inayoongoza kwa uzalishaji wa chakula na kwa mchango wake mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa taifa, na kwamba mkutano huo umefanyika kwa wakati na mahali sahihi.

Ratiba ya mkutano ilijumuisha mihadhara zaidi ya 30, uwasilishaji wa machapisho ya kitaaluma na mijadala ya paneli. Siku ya kwanza ililenga katika suluhisho shirikishi la chakula, nishati na maji, mbinu za umwagiliaji bora na matumizi ya nishati jadidifu katika kilimo. Siku ya pili ilijadili uhimilivu, sera na mnyororo wa thamani kwa mazao kama zabibu, kakao, parachichi, mpunga na mazao ya bustani, na kuhitimishwa na ziara ya shambani pamoja na mafunzo ya vitendo. Siku ya tatu ilijikita katika mbinu za kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi, bioteknolojia, kilimo hai, uwezeshaji wa kijinsia na uboreshaji wa jamii, huku taasisi mbalimbali zikiwasilisha mifano ya mafanikio, ikiwemo Water 4 Mercy na American Jewish Committee.



Washiriki walikubaliana kuwa mkutano huo usiwe tukio la mara moja bali mwanzo wa jitihada za pamoja za muda mrefu. Maazimio yalihusisha kuunda mtandao rasmi wa uratibu, kuanzisha miradi ya majaribio kama umwagiliaji wa kisasa na mnyororo endelevu wa thamani, pamoja na kuanzisha jukwaa la kidijitali la kushirikishana maarifa kwa muda mrefu.
Waandaaji walieleza mkutano huo kuwa ni kichocheo cha kuchukua hatua, wakiweka msisitizo wa kutafsiri mijadala kuwa matokeo yanayopimika. Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini pia ulipendekezwa ili kuhakikisha uwajibikaji na uendelevu wa shughuli.
Mkutano wa FEW Afrika Mashariki ulifungwa Julai 16 kwa wito wa kuendeleza ushirikiano wa kuaminiana na kuimarisha mshikamano wa kikanda. Waandaaji walisisitiza kuwa urithi wa mkutano huu utapimwa sio kwa hotuba za kufunga, bali kwa miradi na hatua zitakazochukuliwa katika miezi na miaka ijayo.



*Prof. Aloys N. Mvuma Makamu Mkuu wa Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) pamoja na Mkurugenzi wa TARI (Tanzania Agricultural Research Institute) wakifurahia wasilisho la Mshiriki kwenye Kongamano la kimataifa la Chakula, Nishati na Maji (FEW) lililoandaliwa na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeyaa Julai 16-16 2025*

# WANACHUO MUST WAHIMIZWA KUONGEZA JUHUDI ZAIDI KATIKA UBUNIFU



*Bi Paschalia Ayubu KERaryo, mwanafunzi wa stashahada ya Usanifu Majengo na Teknolojia ya Majenzi, akitoa ufafanuzi kwa mgeni rasmi Bw. Bundara Mashaka kuhusu ubunifu wake wa jengo linalotarajiwa kujengwa wilayani Mbozi.*

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), kupitia Ndaki ya Usanifu Majengo na Teknolojia ya Majenzi, kiliandaa kwa mafanikio makubwa Wiki ya Usanifu Majengo na Teknolojia ya Majenzi, iliyolenga kuhamasisha ubunifu, utafiti, na uelewa wa kitaaluma katika sekta ya usanifu na ujenzi.

Akiongea katika uzinduzi wa wiki hiyo kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Dkt. Ramadhan Said Tekka aliwasisiza wanafunzi kuwa wabunifu zaidi katika fani zao huku akitanabahisha kuwa katika ubunifu fursa ni nyingi.

katika hatua nyingine Bw. Bundara Mashaka kutoka AQRB, alitoa mada pana kuhusu nafasi ya AQRB katika kuratibu taaluma ya usanifu na ukadiriaji majenzi nchinl na kutoa historia ya bodi hiyo, kazi zake, wajibu wake kwa jamii, na namna ambavyo wanafunzi wanaweza kunufaika kwa kujiunga na bodi hiyo baada ya kuhitimu.
Nae Bw.Paulo S.Kitosi kutoka wizara ya ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi chini aliwasilisha mada juu ya

*"Kurejesha Mustakabali Endelevu na Maeneo Jumuishi ya Mijini"*

ambapo alisisitiza umuhimu wa miji kuwa na maendeleo yanayojali mazingira na yanayowajumuisha watu wa makundi yote. huku akisisitiza umuhimu wa nafasi ya wataalamu wa usanifu majengo katika kuhakikisha miji inakuwa rafiki kwa wote.
Aidha, Bw. Philemone Mwakiwone ndaki ya Usanifu Majengo na Teknolojia ya Majenzi aliwasilisha mada kuhusu umuhimu wa maeneo ya wazi mijini, akieleza kwamba maeneo hayo ni muhimu kwa afya ya jamii, mazingira, na ustawi wa maisha ya watu
Tukio hilo lilihitimishwa kwa kutoa zawadi kwa vikundi vya wanafunzi ambapo mshindi wa kwanza aliondoka na zawadi pesa tasrimu kiasi cha Shiling million moja(1000,000) waliofanya vizuri zaidi katika maonyesho ya bunifu, jambo lililowatia moyo na kuwatambua kwa mchango wao katika taaluma ya usanifu.



# WADAU WA KILIMO NA MUST WAUNGANA KUKUZA UJUZI WA WANAFUNZI KUPITIA MASHAMBA DARASA



Prof. Asheri Mwidege (kulia) akiwa ameketi pamoja na Rasi wa Ndaki ya Insia na Masomo ya Biashara, Dkt. Yohana Sasebo (kushoto), katika picha ya pamoja na wadau wa pembejeo na viwatilifu."

Idara ya Usimamizi wa Biashara – Ndaki ya insia na biashara, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), imeandaa warsha maalum iliyokutanisha wadau wa sekta ya pembejeo, kampuni za mbegu, viuatilifu na mbolea kwa lengo la kuimarisha ushirikiano kati ya chuo na sekta binafsi katika kukuza ujuzi wa wanafunzi. Miongoni mwa makampuni yaliyoshiriki ni YARA, MERU, na East West Seed.

Mratibu wa warsha hiyo, Bw. John Fika Mogha, aliwakaribisha washiriki na kumpa nafasi mhitimu wa Shahada ya Kilimo Biashara kutoka MUST, Bw. Laiza Gidion Andende, kueleza fursa zilizopo chuoni. Bw. Andende alibainisha kuwa MUST imejipanga kuanzisha mashamba biashara yatakayosimamiwa kwa kushirikiana na wadau, ili kutoa nafasi kwa wanafunzi kujifunza kwa vitendo na kuongeza ujuzi unaohitajika kwenye soko la ajira.

Warsha ilifunguliwa rasmi na Prof. Asher Mwidege, Rasi wa Ndaki ya Kampasi ya Rukwa, ambaye alisisitiza umuhimu wa ushirikiano wa vitendo kati ya taasisi za elimu na sekta binafsi. Alibainisha kuwa mashamba darasa yatawasaidia wanafunzi kupata uzoefu wa moja kwa moja katika matumizi ya mbegu bora, mbolea na teknolojia mpya za kilimo, hivyo kuwaandaa kuwa wataalamu na viongozi wa kesho katika sekta ya kilimo.

Kwa upande wa wadau, makampuni yaliyoshiriki yalionesha dhamira ya kushirikiana na MUST kwa kutoa vifaa, mbegu, viuatilifu na utaalamu ili kuhakikisha mashamba darasa yanakuwa na manufaa makubwa kwa wanafunzi. Walisema kuwa ushirikiano huo utasaidia pia sekta binafsi kupata nguvu kazi yenye uelewa na ujuzi unaohitajika sokoni.



Bw. Benson Mulashami Bagwerwa, mwanafunzi wa Ndaki ya Insia na Masomo ya Biashara, akibadilishana mawazo na wadau wa pembejeo na viwatilifu."



*Prof. Asheri Mwidege, mgeni rasmi wa kikao, akitoa maoni kwa wadau wa pembejeo na viwatilifu waliokutana kujadili ushirikiano katika kuendesha mashamba darasa."*


Rasi wa Ndaki ya Insia na Masomo ya Biashara, Dkt. Yohana Sesabo, aliwashukuru wadau kwa utayari wao na kusisitiza kuwa MUST iko tayari kutoa ushirikiano wa karibu kufanikisha mradi huo. Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi, Bw. Benson Mulashami Bagwerwa aliomba warsha kama hizi ziwe endelevu kila mwaka ili kuwapa wanafunzi nafasi ya kujua mwenendo wa sekta ya kilimo na matarajio ya soko la ajira.

Warsha ilihitimishwa huku kila mshiriki akiwa na matarajio makubwa kwamba mashamba darasa yatakuwa nguzo ya ushirikiano wa muda mrefu kati ya MUST na wadau wa sekta ya kilimo. Pia wajumbe walieleza kuwa mradi huo utakuwa chachu ya maendeleo ya kilimo nchini na suluhisho la changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana, kwa kuwapa mafunzo ya vitendo na mbinu bunifu za kilimo chenye tija.

Kwa ujumla, warsha hii imeonesha dira mpya ya ushirikiano kati ya elimu ya juu na sekta binafsi, huku MUST ikibaki mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa nadharia za darasani zinaendana na mahitaji halisi ya kilimo na ajira nchini.



*Bw. Benson Mulashami Bagwerwa, mwanafunzi wa Ndaki ya Insia na Masomo ya Biashara, akibadilishana mawazo na wadau wa pembejeo na viwatilifu."*



# WATAALAMU WA WIZARA YA ELIMU WATEMBELEA MIRADI YA HEET-MUST



*Timu wa wasimamizi wa mradi ya chuo kikuu cha sayansi na teknolojia MUST pamoja na Timu ya wataalamu wa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia ikiongozwa na Eng. Hanington Kagilaki wakiwa kwenye jengo la kituo cha ubunifu na uhaulishaji wa teknolojia*

Timu ya wataalamu kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imefanya ziara ya kikazi katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) Kampasi kuu pamoja na Kampasi ya Rukwa, kwa lengo la kukagua maendeleo ya utekelezaji wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET). Ziara hiyo ni sehemu ya juhudi za serikali kuhakikisha kuwa miradi inayofadhiliwa inatekelezwa kwa kuzingatia viwango vya ubora na malengo yaliyokusudiwa.

Msafara huo wa wataalamu uliongozwa na Eng. Hanington Kagilaki, akiambatana na Arch. Dickson Haule pamoja na QS. Geofrey Nyaluke. Wakiwa chuoni hapo, walitembelea maeneo mbalimbali ya ujenzi yanayohusiana na mradi huo, yakiwemo majengo mapya na miundombinu ya kisasa inayotekelezwa katika Kampasi Kuu ya Mbeya pamoja na Kampasi ya Rukwa.

Katika maeneo yote waliyotembelea, wataalamu hao walishuhudia hatua mbalimbali za ujenzi ambazo zimefikia viwango vya kuridhisha. Majengo hayo yanatarajiwa kutoa mchango mkubwa katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, na hivyo kuongeza ubora wa elimu inayotolewa chuoni hapo.

Uongozi wa Chuo, ukiongozwa na Makamu Mkuu wa Chuo pamoja na viongozi wa vitengo mbalimbali, uliwapokea wageni hao kwa ukarimu mkubwa. Katika mawasilisho yao, walitoa taarifa ya kina kuhusu mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mradi, changamoto zilizojitokeza njiani, na mikakati iliyowekwa ili kuhakikisha mradi unatekelezwa kwa mafanikio.



*Ndugu Iman Mwalumbwe Mkurugenzi wa TEHAMA Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (wapili Kushoto) akitoa maoni kwa mkandarasi kuhusu miundombinu ya TEHAMA*



Qs. Dr. Japhary Shengeza kutoka Chuo kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya akitoa maelezo kwa Qs. Geofrey Nyaluke (Wapili Kushoto) kutoka Wizara ya Elimu Sayansi

Akizungumza kwa niaba ya timu ya wataalamu, Eng. Kagilaki alieleza kuridhishwa na kasi ya utekelezaji wa mradi na ubora wa miundombinu inayojengwa. Alitoa pongezi kwa uongozi wa chuo kwa kusimamia vyema miradi hiyo na kusisitiza umuhimu wa kuendeleza ubunifu, uwajibikaji, na ushirikiano ili kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa.



Timu ya wataalamu kutoka Wizara ya elimu Sayansi na Teknolojia ikiwa pamoja na timu ya usimamizi wa mradi wa HEET Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya wakiwa kwenye mjadala wakati wa kukagua maendeleo ya mradi



Timu ya Ukaguzi wa Mradi ikiwa pamoja na Wataalamu wa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia sambamba na mkandarasi wa Mradi wakibadilishana Mawazo ili kuboresha majenzi



Timu ya Ukaguzi wa Mradi ikiwa pamoja na Wataalamu wa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia sambamba na mkandarasi wa Mradi wakibadilishana Mawazo ili kuboresha majenzi

Kwa upande wake, Arch. Haule alisisitiza umuhimu wa matumizi bora ya rasilimali na kuhakikisha kuwa kila kipengele cha usanifu kinazingatia viwango vya kitaifa na kimataifa. Naye QS. Nyaluke alitoa ushauri kuhusu udhibiti wa gharama na ufanisi wa matumizi ya bajeti.

Mradi wa HEET unalenga kuimarisha elimu ya juu nchini kwa kuwekeza katika miundombinu, vifaa vya kufundishia, utafiti na maendeleo ya kitaaluma. MUST ni miongoni mwa taasisi za elimu ya juu zinazofaidika na mradi huu, ambao unatarajiwa kuleta mageuzi chanya katika mfumo wa elimu na hatimaye kuchangia maendeleo ya kiuchumi ya taifa.

Kwa ujumla, ziara hii imeonesha mshikamano kati ya serikali na taasisi za elimu ya juu katika kuhakikisha malengo ya kitaifa ya maendeleo ya elimu yanatimia kwa vitendo.



Ndugu Iman Mwalumbwe Mkurugenzi wa TEHAMA Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (wapili Kushoto) akitoa maoni kwa mkandarasi kuhusu miundombinu ya TEHAMA

# WIKI MENEJA 2025 YAWAVUTIA WENGI



*Dkt. Emmanuel Tonya (wa pili kutoka kulia) akiwa na mgeni rasmi wa Siku ya Meneja (aliyeketi katikati) pamoja na Mkuu wa Idara ya Usimamizi wa Biashara, Dkt. Lazaro Edward Kagata, wakifuatilia Uwasilishaji wa Mipango ya Biashara kutoka kwa wanafunzi wa Ndaki ya Insia na Masomo ya Biashara.*

Kilele cha Siku ya Meneja kilichoratibiwa na Ndaki ya Insia na Masomo ya Biashara katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), kimefanyika kwa mafanikio makubwa, kikilenga kuinua fikra za wanafunzi kuhusu uongozi, ubunifu na ujasiriamali.

Akizungumza katika kilele hicho kaimu makamu mkuu wa Chuo Dr.Ramadhan Tekka aliwataka wanafunzi kuchangamkia fursa zinazojitokeza chuoni ikiwa ni pamoja na kushiriki matukio malimbaliyatakayowasaidia kujenga ujasiri, kuimarisha uelewa nakupata ujuzi wa maisha halisi.

katika kilele hicho pia Ndaki ilimualika Mhandisi Bugalama kuwa miongoni mwa wageni maalumu, akizungumza na wanafunzi mhandisi Bugalama aliwahimiza wanafunzi kutumia vyema muda wao wakiwa Chuoni na kusisitiza kuwa chuo si mahali pa kusoma tu vitabu bali pia ni jukwaa la kujifunza maisha.

Katika kilele hicho, wanafunzi walipata fursa ya kuwasilisha mawazo yao ya kibiashara mbele ya majaji na wageni mbalimbali. Baadhi ya mawazo yaliyowasilishwa ni pamoja na, Uchoraji kwa kutumia uzi, Tafiti na Mashine ya kutotolesha mayai kwa gharama nafuu



*Rasi wa Ndaki ya Insia na Masomo ya Biashara, Dkt. Emmanuel Tonya, akimkabidhi cheti cha pongezi mgeni rasmi, Mhandisi Bugalama Kulwa, katika kilele cha Wiki ya Meneja."*

Mwanafunzi Joseph Nelson aliibuka mshindi wa kwanza baada ya kuwasilisha wazo la mashine ya kutotolesha mayai, wazo ambalo ni la kibunifu na linatekelezeka ubunifu huu ni mfano mzuri wa jinsi wanafunzi wanavyoweza kubuni suluhisho za changamoto za kijamii na kiuchumi.



*Kaimu Mkuu wa Chuo"Dkt. Ramadhani Tekka akizungumza katika hafla ya ufunguzi wa kilele cha wiki ya Meneja iliyoandaliwa na Ndaki ya Insia na Masomo ya Biashara*

Ndaki ya Insia na Masomo ya biashara ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) huandaa maonesho mbalimbali kila mwaka huku wakionesha bunifu mbalimbali na shughuli mbali mbali za kijasiliamali ambazo hufanywa na wanafunzi wa ndaki hiyo.



*Wanafunzi walioshiriki Wiki ya Meneja wakifuatilia kwa makini uwasilishaji wa mipango ya biashara kutoka kwa wenzao ndani ya Ukumbi wa Nyerere.*

# WARSHA KWA VIONGOZI WA CHUO KUKUZA UWAJIBIKAJI, WELEDI NA UMOJA



*Prof. Aloys Mvuma (Makamu Mkuu wa Chuo) akiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi mbali mbali wa chuo mara baada ya kuhitimisha hafra ya Warsha.*

Mpango wa Mafunzo kwa Viongozi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) ulizinduliwa rasmi tarehe 8 Machi 2025 na kukamilika kwa mafanikio mnamo tarehe 12 Julai 2025. Mpango huu wa kimkakati uliandaliwa kwa lengo la kuimarisha uwezo wa uongozi ndani ya chuo, kukuza ushirikiano baina ya vitengo mbalimbali, na kuoanisha mbinu za usimamizi na dira pamoja na dhamira ya taasisi.

Kwa kipindi cha miezi minne, mafunzo haya yaliwaleta pamoja viongozi 82 kutoka ngazi mbalimbali za uongozi wa chuo, wakiwemo viongozi wapya walioteuliwa na wale wenye uzoefu wa muda mrefu. Malengo yake yalikuwa mapana lakini yanayohusiana kwa karibu: kujenga mshikamano na kazi ya pamoja, kupunguza mipaka ya kihairakia kati ya wasimamizi na walio chini yao, kuboresha mawasiliano ya ana kwa ana na ya kijamii, na kuziba pengo kati ya majukumu ya uongozi na usimamizi. Vilevile, mpango huu mafunzo ulilenga kuwajengea viongozi wapya uelewa wa mifumo ya utawala na sera za chuo, kuwezesha kubadilishana mawazo, na kuimarisha imani ya pamoja kwamba hakuna kiongozi kamili au bora kabisa, bali viongozi bora ni wale wanaoendelea kukua kupitia kujifunza, ushirikiano, na tafakuri endelevu.



*Viongozi mbali mbali wa chuo wakifuatilia wasilisho wakati wa Warsha.*



*Prof. Aloys N. Mvuma (Makamu Mkuu wa Chuo) akifafanua jambo kwa viongozi wakati wa Warsha.*

Mafunzo haya yalitumia mbinu shirikishi zilizojumuisha, mijadala, uchambuzi wa visa halisi (case studies), pamoja na maswali na majibu. Njia hizi zilihamasisha mawasiliano ya wazi, utatuzi wa changamoto kwa pamoja, na kujifunza kwa pande zote. Kupitia mijadala, washiriki waliweza kujenga uaminifu na kuelewana zaidi, hivyo kuimarisha stadi zao za kitaalamu na mahusiano kazini.

Watoa mada kutoka ndani na nje chuo waliwaongoza washiriki kupitia mada nyingi zenye umuhimu mkubwa kwa uongozi wa taasisi za elimu ya juu. Vipindi vya utangulizi vilivyoongozwa na Profesa Godliving Mtui vilichunguza "Kiini cha Uongozi na Usimamizi" pamoja na "Misingi ya Uongozi na Usimamizi," akisisitiza umuhimu wa mawasiliano bora, ugawaji wa majukumu, uongozi wa kimkakati, na usimamizi wa mabadiliko. Vipindi hivi vya utangulizi vilitoa msingi imara kwa awamu zilizofuata, vikichanganya nadharia na matumizi halisi.



*Prof. Godliving Mtui akimkabidhi cheti cha ushiriki Prof. Aloys N. Mvuma (Makamu Mkuu wa Chuo).*

Kadri mafunzo yalivyoendelea, mada zilipanuka kujumuisha uongozi wa kitaaluma, utawala wa maadili, na uhakikishaji wa ubora; kuhamasisha washiriki kudumisha uwajibikaji, umoja, na ubunifu katika majukumu yao ya uongozi. Mnamo mwezi Aprili, Wakili Lugano Mwakilasa aliongoza warsha ya kuvutia kuhusu Utawala wa Vyuo Vikuu, akifafanua mifumo ya kisheria, ikiwemo MUST Charter na sera husika za kitaifa. Mada hizi zilienda sambamba na mada za usimamizi wa fedha na mipango ya kimkakati, zilizoangazia uwazi, nidhamu ya kifedha, na matumizi ya mifumo ya kitaifa kama GAMIS, GePG, na PlanRep.



*Makamu Mkuu wa Chuo - Prof. Aloys N. Mvuma (katikati - mbele) akiwa kwenye pcha ya pamoja na Prof. Said Vuai - DVC ARC (kulia), Prof. Zacharia Katambala - DVC PFA (kushoto) na Prof. Godlingi Mtui (aliye simama)*

Hata hivyo, Baadaye wataalamu katika elimu jumuishi, usimamizi wa TEHAMA, usimamizi wa majengo, manunuzi, na usimamizi wa rasilimali watu, wakiongozwa na Dkt. Magreth Matonya kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, na Bw. M. Masanja kutoka Kurugenzi ya Utawala na Rasilimali Watu walitoa somo kwa viongozi. Huku mada hizi zikisisitiza umuhimu wa ujumuishi, mabadiliko ya kidijitali, na ufanisi wa shughuli za taasisi kupitia matumizi ya mifumo kama PEPMIS, e-Office, na e-Mrejesho.



*Makamu Mkuu wa Chuo - Prof. Aloys N. Mvuma akimkabidhi cheti cha ushiriki Prof. Zacharia Katambala - DVC PFA*



Makamu Mkuu wa Chuo - Prof. Aloys N. Mvuma akimkabidhi cheti cha ushiriki Prof. Said Vuai DVC - ARC

Katika muda wote wa vipindi kumi na tatu vilivyofanyika, ushiriki wa washiriki ulikuwa wa kiwango cha juu na thabiti. Kati ya viongozi 82 waliokuwa wamejiandikisha. Hii ni ishara ya ari na dhamira yao ya kujenga uwezo wa kitaalamu. Hali hii ya ushiriki mkubwa ilionyesha umuhimu wa warsha hii na athari chanya iliyoleta katika kukuza utamaduni wa uongozi ndani ya MUST.

Warsha hii ilifungwa rasmi tarehe 12Julai 2025 kwa hafla ya utoaji vyeti kwa washiriki wote waliokamilisha mafunzo. Hafla hiyo ilihudhuriwa na Makamu Mkuu wa Chuo, Profesa Aloys N. Mvuma, ambaye alikabidhi vyeti kwa mshiriki, kama ishara ya kutambua juhudi na ushiriki wake wa dhati. Katika hotuba yake ya kufunga, Profesa Mvuma aliwapongeza viongozi hao kwa kujituma na kujifunza kwa bidii, akisisitiza imani ya chuo katika uwezo wao wa kuongoza kwa maadili, maono, na ushirikiano.



Makamu Mkuu wa Chuo - Prof. Aloys N. Mvuma (katikati - mbele), Prof. Said Vuai - DVC ARC (kulia), na Prof. Zacharia Katambala - DVC PFA (kushoto) wakiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi mbali mbli.



Prof. Godliving Mtui akipokea cheti cha ushiriki kutoka kwa Makamu Mkuu wa Chuo - Prof. Aloys N. Mvuma

Kwa kuhitimisha warsha hii, washiriki waliondoka wakiwa na imani mpya, uelewa mpana wa uongozi bora, na mshikamano ulioimarishwa kati yao kama timu ya uongozi. Warsha hii imeweka msingi thabiti wa kuendeleza utamaduni wa uongozi unaojikita katika uwajibikaji, ushirikiano, na maono ya pamoja ; utamaduni unaoiwezesha MUST katika kufikia ubora wa kitaaluma na ufanisi wa taasisi.



Prof. Asheri Midege Rasi Ndaki ya Rukwa akifuatilia Warsha pamoja na viongozi wenzake.



Makamu Mkuu wa Chuo - Prof. Aloys N. Mvuma (katikati - mbele), Prof. Said Vuai - DVC ARC (kulia), na Prof. Zacharia Katambala - DVC PFA (kushoto) wakiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi mbali mabli.



## Mawasiliano zaidi :


Fax : +255 (0) 25 2957552

Tel : +255 (0) 25 2957540/4 | +255 (0) 25 2957540/2

S.L.P 131 Mbeya - Tanzania

Email : vc@must.ac.tz